BINT EL SUDAN
Perfume * Powder
Pomade * Deodorant
MARASHI
ASILI YA MAPENZI
HAKIKA
UTA FURAHI

Waimbaji Kutoka Dar Watumbuiza Msa

PWANI ilipata bahati kubwa kwa kutembelewa na kikundi cha waimbaji mashuhuri wa nyimbo za Twaarab kutoka Dar es Salaam, Tanzania kinachojulikana kama El-Wattan Musical Club ambapo waliwatumbuiza wananchi kwa nyimbo za kuvutia mjini Mombasa kwenye hafla mbali mbali.

Chama hiki cha El-Watan kina waimbaji wa nyimbo za Twarab, ambazo kwa kawaida huwavutia wote wale wanaongea Kiswahili, hasa wakaazi wa sehemu za Pwani ya Afrika Mashariki.

Twarab ni mtindo maalumu wa nyimbo za Kiswahili na ala zake ni za aina kutoka utamaduni wa Ki-magharibi, Mashariki ya Kati na Bara Hindi na pia Uswahilini.

Twarab ni mtindo wa nyimbo za kuvutia sana kwani huwa zina maelezo ya kudidimia juu ya jambo ama fumbo fulani linaloimbiwa. Mwimbaji hutumia sauti yake ya kupendeza na kuvutia ili awe na uwezo mkubwa zaidi wa kufikisha ujumbe uliomo katika nyimbo hiyo anayoimba.

Kwa miaka mingi sasa mtindo wa uimbaji wa Twarab umechukua jukumu la kueneza mwengozo wa siasa katika nchi kama vile Tanzania na Somalia, na katika nchi hizo kuna vyama vya Twarab vinavyongozwa na Serikali yenyewe.

Kwa mfano, Somalia kuna mwimbaji maarufu, Bi Asha Abdo, maarufu anaitwa "Malika" ambaye nyimbo zake za siasa na mapenzi zinatumiwa katika Idhaa kadha wa Kadha katika Ulimwengu kama vile BBC, Radio China, Radio Cairo, Radio Tanzania na hata mara nyingine husikiwa katika Idhaa ya Kiswahili ya Sauti ya Kenya.

Jambo la kusikitisha ni kuona katika mwanzo wa miaka ya hamsini Pwani ya Kenya ilikuwa na vyama mashuhuri sana vya Twarab kama vile vya Johar Ochestra na Morning Star.

Vyana hivi vilikuwa vina vifaa kamili vya uimbaji na vikipendeza mno sie tu katika Pwani ya Kenya bali sifa zao zilifika hadi huke Unguja.

VYAMA hivi na vinginevyo vidogo vyao vilipata kutiwa nguvu sana pale *"Sauti ya Mvita* ilipokuwa Mombasa, chini ya uwongozi wa Sheikh Hyder na Bw. Hunt hadi wakati wa Bw. Pitchford na Bw. Webb.

Wazungu hawa walikuwa walishirikiana na Sauti ya Unguja hasa katika ubadilishanaji wa vipindi vya nyimbo za Twarab.

Jambo hili liliwatia ghera waimbaji wa Twarab wa Pwani ya Kenya na kamwe kutokubali kushindwa na chama chochote kile hata maarufa cha Unguja kilichokuwa na mabingwa kama vile Bi. Maryam na Bwana Bakari Abeid ambaye kwa miaka mingi sana jina lake lilivuma katika uimbaji wa Twarab.

MNAMO mwezi wa Septemba, mwaka huu chama cha El-Watan kilikuja Mombasa na kuwatumbuiza wananchi. Mashabiki wa Twarab walifurahiwa na kuvutiwa na nyimbo zao muruwa.

Safari yao ya mwezi wa September ilifana na kufaulu vizuri na hata wao wenyewe walitoa shukrani kwa upokeaji wa kikarimu waliopata kwa wakaazi wa Mombasa.

• **HABARI hii imeandikwa na *FARAJ DUMILA,* mwandishi maarufu wa mambo ya utamaduni.**

• *MARYAM MOH'D*

• *MOZA ALI*

• *MTUMWA RAJABU*

ZILIPENDWA! REX FC

LEO TUNAWALETEA ukumbusho mkubwa kwa wanasoka wa pwani kwani wanandinga hawa kama wanavyojieleza kwenye mpira ni wa timu ya Rex ambayo ilikuwa chanzo cha kuanzishwa kwa timu ya Feisal pamoja na timu za Young Bondeni na Game By Force. Waliosimama kutoka kushoto ni Mahmood Salim, Marehemu Ahmed Abubar, Barazanji, Leonard Hammond *Leni,* **Marehemu Olunza** *Bongo Baba* **na Shariff Kimwinyi. Waliokaa vitini ni Hyder** *Madagascar,* **Imu Antar, Marehemu Maamun rashid, Marehemu Kibwana** *Wembley,* **Mwalimu Joseph Stephens. Waliolalal chini ni Marehemu Jumanne** *Bajack* **na Muu Naaman (kulia) ambaye ndiye aliyetuletea picha hii.**

Karibu Siku Ya Jamhuri

Bisimilahi awali
Rabi une taka bali
Duwa iwe makubuli
Kwa Salama na afuwa

Jamhuri mewa sili
Wa karibu na wambali
Furaha ya kilahali
Kwa salama na afuwa

Jamhuri ni Jamali
Liwalo kwetu salhali
Madawa na maakuli
Kwa salama afuwa

Makaririya jalali
Kipenzi chetu halali
Raisi hilo habari
Kwa salamana afuwa

Baiti tano kalili
Sileo toka ghazali
Maendeleo kamili
Kwa salama na afuwa

Rabinaio mba duwa
Mikono nimeenu wa
Nipate kufurahiwa
Jamhuri mewa sili

Kwa salama na afuwa
Na sote twa furahiwa
Na Kenya Twapendezewa
Jamhuri mewasili

Ndugu leo na tongowa
Kenya tume jaaliwa
Yote tusha barikiwa
Jamhuri mewasili

Moyoni sina ukiwa
Kwa Juhudi twamjuwa
Huduma twa hudumiwa
Jamuhuri mewasili

Lakini ni mari dhawa
Jamhuri ya chanuwa
Shukurani nazi towa
Jamhuri mewasili

USTADH AHMAD MATANO,
MOMBASA

MASHAIRI haya juu ya Sikukuu ya Jamhuri tumeletewa na Mshairi Maarufu kutoka Majengo ya Mussa, Mombasa. Ustadh Ahmed Matano Kipachu (pichani juu).

Siku Ya Wazazi

MBUNGE wa Mombasa Kusini, Bw. Abdallah Ndovu Mwidau akimpongeza mmoja wa washindi wa uchoraji kutoka Shule ya Msingi ya Alibhai Panju wakati wa sherehe ya siku ya wazazi katika shule hiyo.

PICHA: CAESAR MADDANGANHA

Apenda Kuogelea Kwenda Sinema

MPIGAJI picha maarufu jijini Mombasa, Bw. Caesar Maddanganha alikumbana na msichana huyu wa miaka 18, bi. Rahab Ali katika pata-shika yake ya kutafuta yale yatakayowapendeza wasomaji. Lakini dada katu akakataa kueleza chochote juu ya maisha yake. Bi. Rahab alisema: "Sina haja ya kukwambia mengi isipokuwa napenda kuogelea, kwenda sinema na kusoma COASTWEEK.

PICHA NA STORI: CAESAR MADDANGANHA

• *RAHAB ALI*

Farucci
BINT EL SUDAN
Perfume * Powder
Pomade * Deodorant
MARASHI
ASILI YA MAPENZI
HAKIKA
UTA FURAHI

JISHINDIE VIATU MARIDADI VYA FARUCCI KWA MSHINDI WA KWANZA NA 'BINT EL SUDAN

GIFT PACK' KWA WASHINDI WA PILI NA WATATU KATIKA SHINDANO JIPYA LA KUJAZA MANENO

CROSSWORD No. 200

KWENDA KULIA:

1. Namna ya samaki wa mtoni auziwani. 5. Serikali ya Kenya. 6. Chagura. 7. Wakati wa asubuhi. 8. Ama. 9. Nchi huru Afrika. 11. Mchezo wa kitoto. 12. Jenga. 13. Shika amri. 15. Sielewi, sifahamu. 16. Si ile. 17. BAA.

KWENDA CHINI:

1. Mahali penye miti mifupi na nyasi. 2. Eneo la duni lenye maji. 3. Kula kwa ulimi. 4. Aina ya mmeakama mnazi. 7. Mtumbaya. 10. Pambo la kike. 11. Chombo cha kulazia nguo. 13. Weka ndani. 14. Isipokuwa.



JINA.......................................

SANDUKU LA POSTA..........................

....

MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO NO. 199

KWENDA KULIA: 1. EVEREST, 5. AM, 6. TONE, 8. WAZIMU, 10. ISA, 11. PEA, 12. AMINA, 14. MBA, 16. MBALE, 18. LEO, 19. LO. *KWENDA CHINI:* 1. ELEWA, 2. RAMISI, 3. TEO, 4. NGE, 5. AZIMIA, 6. TU, 7. NYEMBE, 9. MANDE, 13. AMI, 14. MLO, 15. AOA, 17. LA.

WASHINDI WA FUMBO LA KUJAZA MANENO No. 199

1. Hassan Ariff, Sanduku La Posta 88433, Mombasa. 2. Yahya Salim Sanduku La Posta 81615, Mombasa. 3. Aidarus Hussein Maulana Sanduku La Posta 98639, Mombasa.

Shindano la Fumbo la Kujaza Maneno:—

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yetakayokubaliwa. Washindi watatu kila baada yawiki mbili watapata viatu na 'Bint El Sudan - Gift Pack'. Shindano hili limedhaminiwa na *COASTWEEK* limited Mombasa. Jawabu za fombo hili lipelekwe kwa Mhariri *COASTWEEK,* Sanduku la Posta 87270, Mombasa, Kenya. Siku ya jumatano tarehe **Dec. 26 1984** saa, nne asubihi shindano hili litakuwa mwisho.